

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

MARAKWET WEST CONSTITUENCY

AT KAPSOWAR GIRLS SECONDARY SCHOOL

ON

Friday, 28th June, 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MARAKWET WEST CONSTITUENCY HEARING HELD AT
KAPSOWAR GIRLS SECONDARY SCHOOL ON 28th June, 2002 AT 11.20 AM.**

Present

Com. Domiziano Ratanya - In the Chair
Com. Riunga Raiji
Com. Salome Muigai

Secretarial Staff in Attendance

John Watibini - Program Officer
Lyme Sigei - Assistant Program Officer
Grace Gitu - Verbatim Reporter
Solomon Kibet Cheserek - District Co-ordinator

Com. Domiziano Ratanya: Tungetaka kuona kwamba tunaanza nimesikia watu wako hapa ??? na watakuja. Kwa hivyo kwa wale ambao wamefika tungeweza kuendelea. Na ningetaka kuwajulisha hiki ni kikao cha Constitution of Kenya Review Commission na tumekuja kusikia maoni yenu kuhusu kubadilisha Katiba. Na kwanza sasa kungojea wengine wakati wanaweza kuingia lakini kabla ya kufanya hivyo ningetaka kwanza tuombe Mungu atukubalie na atupatie nguvu ya kuendelea na kazi yetu. Kama kuna pastor yeyote anaweza kuendesha maombi.

Pastor: Haya tuombe pamoja. Mungu wetu aliye mbinguni, muumba wa watu wote, Mungu anayetupenda, anatupatia mvua, anatulinda kwa safari yote, Mungu mwenye kuunda serikali hapa tunakuja mbele zako asubuhi hii tukikushukuru vile umetuongoza mpaka tumekutana kwa hii nyumba ili tuangalie mambo ya Katiba ya nchi yetu. Asante kwa wale umeleta kutoka mbali na sisi ambao tumetoka karibu Mungu tunakuomba utuongoze sasa kwa mazungumzo yote. Asante kwa roho wako ambao anaongoza watu na kutupatia mawazo safi, Mungu tusaide kama watu wa Marakwet ili tuwaze vizuri juu ya Katiba tuangalie mambo yote ambayo unaweza kutusaidia. Tukianza kikao hiki anza pamoja na sisi Mungu wetu mpaka mwisho. Wale wako njiani uwalete, uwaharakishe ili tushikane pamoja kwa ushirika. Tuongoze na utubariki kwa sababu tunaomba kwa jina la Yesu aliye mwokozi wetu. Amen. Asante.

Com. Domiziano Ratanya: Asante sana pastor, sasa tungetaka kuwajulisheni wale ambao tunaotoka kwa Commission, Commissioners wenyewe na sub-commissioners ?? Na hapa niko upande wangu wa kulia hapa ni Commissioner Riunga Raiji ambayo saa ingine atasema baadaye na upande wangu mwingine kuna Commissioner Salome Muigai. Tuko Commissioners watatu kwa hii panel na members wetu kutoka kwa ofisi yetu tuna John Watubiri –Program Officer, huyu ndiye anasimamia

staffs ambao tumekuja nao kama Program officer kwa hii tume yetu, then kuna Lyme Sigei, Assistant Program officer huyu ako hapo, anasaidia na tuna mwingine Grace Gitu wa recording. Yaani hapo mkiangalia mtaona hio ka-recorder ya kunasa sauti yako wakati unapeana maoni yako. Na hapo hapo ningewauliza wakati unapeana maoni uzungumze kwa hio kitu mnaona hapa – kipasha sauti ili sauti yako nayo iende kwa machine yenyewe.

Ee sasa kitu kingine kabla ya kwanza ningetaka tukubaliane mipango, mpango mwenyewe wa kuendesha mkutano wetu wa leo. Kwanza kwa lugha, lugha kama ungetaka kuongea lugha yote ya kitaifa kama Kiswahili ama Kiingereza, una uhuru wa kufanya hivyo. Kama umeandika maandishi yako kwa Kiingereza ama Kiswahili unaweza kufanya hivyo na hata lugha ya kienyeji, kama huwezi kuongea kiingereza au Kiswahili unaweza tumia lugha a kienyeji na tutakuwa na mtu wa kutuambiwa vile inasema.

Tena hii list mnaona hapa, ni majina yenu yameandikishwa na nitafuate kama vile imeandikwa kutoka kwa kwanza napatia wa pili, hakuna kuruka lakini kama tutakuwa na sababu yeyote ya kuruka – Commissioners wanaweza kuamua, kwa mfano, kama mama akija ambaye ni mzee sana ama baba mzee sana na hatutaki kumueka sana ama mama mzito aje na hatuwezi kumuweka, hata ingawa amekuja nyuma yako, tungeweza kumuita. Hivi tutatumia mamlaka yetu. Ama kama mtoto wa shule, amekuja apeane maoni yake na arudi katika classroom kuendelea na masomo, hata huyo tungepatia nafasi lakini tutaendelea kufuata hii.

Hio ni kitu muhimu na kingine mambo ya kupeana maoni yenyewe – yule ambaye atapeana maoni atakuja hapa akiwa na maandishi, hiyo ndio tunaita Memorandum, maandishi ambayo ameandika atapeana tu yale ya muhimu katika hiyo maandishi, hatuwezi kubaila mtu kuchukua karatasi asome memorandum kwa sababu hio itakaa wakati mrefu na tena si kazi ya leo. Memorandum tunapeleka ofisi, inasomwa, inakuwa analysed na maneno yako yote inaandikwa vizuri. Kwa ile memorandum usiendeleo kusoma kwa sababu saa ile nitakupatia haiwezi kubali usome ni kutaja ile ya muhimu tu. – highlight. Na halafu utupatie memorandum iwekwe hapa na tukirudi ofisi tutaendelea kuangalia mambo yako.

Now, kama mtu hana memorandum, kuongea tu kwa mdomo hata hiyo ni njia ingine ya kuongea kwa masaa yale utapewa nitakwambia hapo unaongea na kutoa mambo yako. Na kama una memorandum tena, na hutaki kuzungumza, hutaki kuongea kabisa kusema lolote, unaweza kwenda upeane pale kwa officers wetu, u-sign na iandikwe na ukitaka kuketi uzikilize wengine, una uhuru wa kufanya namna hiyo au ukitaka kwenda kabisa una uhuru wa kufanya hivyo, hioni njia ingine. Kwa hivyo mkumbuke hizo njia tatu, kwa maandishi utapeana kwa ufupi, na halafu, maneno ya mdomo na memorandum ambayo unataka kuweka, iandikwe pale na uende bila kuzungumza, hiyo inakubaliwa.

Kitu kingine ningetaka kumwambia mwanzoni in kwamba hii Commission ni Commission ambayo imepewa mamlaka ya kuchukua maoni ya wananchi kila pahali katika Kenya. Na hapa tumefika Marakwet Constituency. Tulikuwa jana Ukwalo na sasa tuko hapa.

Uko huru kupeana maoni yako bila kuogopa. Kwa sababu hayo ni maoni yake ambaye atasaidia kurekebisha Katika yetu. Kwa hivyo usije ukaogopa yeyote kuogopa pengine chief ama yeyote, tunasema ni maoni yako na uhuru wa kusema maoni yake. Kwa hivyo hapo msiogope.

Na tena nimewambia kwamba ukipewa nafasi yako masaa yale nitakupatia ni dakika tano, - 5 minutes. Ukimaliza hiyo dakika tano nitakwambia saa imekwisha; kama ningekuwa na kengele hapa pahali pengine tunapiga kengele kama iko napiga kidogo hapa, unasikia na unamaliza. Sababu ukiendelea kuchukua nafasi zaidi, utapotelea wengine wakati kwa hivyo hapa tuheshimiane kabisa. Dakika zako zikiisha tano, umalize, utupatie memorandum yako, na uende pale u-sign register yetu. Na nitashukuru sana kama utakubali hivyo. Tunakubaliana hapo! Dadika ngapi? Tano, kwa hivyo sikusikia anayesema sita, ni tano. Kwa hivyo ukipitisha tano, umekosea hawa wananchi wote na wale watakuja baadaye pamoja na sisi.

Sasa bila kupoteza wakati mwingine eeh, kitu kingine ningependa kuwakumbusha ni kwamba kama ukimaliza kuzungumza, Commissioner yeyote hapa akiwa na kitu cha kuuliza swali ama kufafanua kitu fulani, anaweza kufanya hivyo yaani kuliza ungoje akulize maswali ama ufafanusi wowote.

Sasa nitaendelea kuanzia mtu wa kwanza ee , Joel Kibet Chebor.

Joel kibet Chebor: Mwenyekiti wa Kamati hii waliofika hapa leo na pia wenzangu hatukujirishwa ya kwamba tutakuwa na mkutano leo na leo ndio ??? na yangu ??? niwashukuru sana sana kusikia maoni yetu . Mimi maoni yangu, jina langu Joel Kibet arap Chebor. Maoni yangu sisi hatukufindishwa kama vile iliambiwa ya kwamba kuna wale ambao wanatembezwa wanapewa pesa na kuendelea kuonyesha watu ya kwamba ?? sisi hatujui leo Katiba hii ni ya aina gani. Sisi zamani tulikuwa na Katiba ya utamaduni kama tumeitwa na wazee wamekata shauri hio maneno inafuatwa.

Pili katika nchi yetu hii kila mtu alikuwa na sehemu yake na ilikuwa inaheshimiwa sana. Hapana mtu kwenda kuchukua la mwingine na kunyanyasa wengine. Sisi nataka Katiba hii ya leo ya kwamba inaheshimu mtu na mali yake ata kwa njia yao yenyewe, sisi ni nchi ya kutosha. Hata Bwana mwenyekiti unaona msitu ni kubwa sana. Kuna wengine hawana msitu na walikuwa wanaomba wale wenye wako na msitu na walikuwa napewa.

Na sisi, leo nataka Katiba ya kulinda sisi, hata wale watu wachache tulindwe.Hata mali yao. Na Katiba hio iwe namna hiyo na wala si ya kunyang'anya wengine.

Pili, mimi kwa wale ambao wako kwa kazi unaambiwa kwa kazi we unajua Katiba hii ya kiandikwa wengine, wengine wananyanyasa wengine, wengine wananyanyasa wengine. Kwa hivyo tunataka Katiba ya kufuata wale wengine wasio kuwa na elimu na wana elimu wafuatiwe. Wapatiwe nafasi, nafasi. Bwana mwenyekiti mimi sitaki kuongeza mengi sababu unasema dakika yangu imepita karibu dakika tano inabaki dakika mbili. Basi mimi naona ya kwamba yangu inatosha hapo tu

yakuangalia Katiba yetu ya kwamba turekembishe Katiba, tunataka Katiba ambayo inakubaliwa na watu wote.

Pili tunataka watu watufundishe sio kama leo wanakuja siku moja wanasema Katiba inakwenda “bambam” apana. Kwa wale waliotumwa, waje watufundishe. Asante.

Com. Domiziano Ratanya: Asante sana Joel Kibet kuja hapo kidogo, okey nenda pale uandikishe na asante sana kwa kutumia masaa lakini umebakisha dakika tatu lakini umemaliza mapema, asante sana. Ee kuna Christine Talaam, Christine Talaam.

Christine Talaam: Commissioners, ninawakaribisha hapa district yetu Marakwet, mimi ni Christine Talaam, Maendeleo ya Wanawake Organisation, nasimamia akina mama katika district hii. Vile tumekutana na akina mama wa division tulipata 49 points ya kusema leo na kunakutanisha na vile tulifanya kwa division tulikuwa na more than 65 attendants from location, sub-locations na tulifikia wote na wametupatia maneno yao yote tuko nayo tunaandika, tumekutanisha na kwa sababu umeleta tu nafasi kidogo niko na secretary atakuja kusoma na kabla hajakuja ningesema asante kwa sababu hii watu wa Commissioners wamechanganya, tuko na gender, wamama kama mimi, sasa hio maneno yetu tukisoma wakina mama muweke sawa kitu ya maana kwa sababu mnatu-represent hapo. Sasa mtaona hata mahali tumekosea kidogo, msahihishe. Na sitaendelea kusema maneno mengi nitaita secretary yangu ya Maendeleo ya Wanawake Organisation of which aseme kile tumeandika. Asanteni.

Com. Domiziano Ratanya: Asante Christine, secretary wako sasa ataendelea kutupatia yale ambayo mmeandika. Kwa jina unaitwa –

Lydia Kanda: Naitwa Lydia Kanda. Vile tumeandika, tumeandika kwa lugha ya kimobo na kama vile mwenyekiti amesema tulipata maoni 49 nitasema tu kumi hivi kwa sababu ya saa.

Bwana Commissioner, tulipata kuwa wamama walisema

1. Justice to be available in the Constitution.
2. Women to be recognised in the community in the new constitution. I can explain this abit women in Marakwet are not seen as people. So they are called children . So women decided to be recognised in the new Constitution as human beings. Firstly they said women to be recognised as adults. Men and women equality in the Constitution to be changed. Also good customary law to be incorporated in the national Constitution.
3. Another one is the murder cases or killing. The concerned mothers should be prosecuted without involving relatives.
4. Also they said land ownership women, men and children to be equal on land ownership in the national Constitution.

5. Also they said legal customary law, e.g. forced marriages should be changed and stopped immediately.
6. Also the customary law to be under the national Constitution but to be legalised to be seen as any other marriage and issue of certificate to be sealed.
7. On early pregnancy of girls, the new Constitution should involve both the girl and the boy in stealing because you can see girls are just left that way and the boys are free. A girl can be sent away from school and the boy will be admitted and left to continue with his education. Therefore we want the girl/ boy to be the same.
8. Kenyan Constitution to be reached easily by all the people e.g. local libraries, chief for easy references.

I think because of time, I will stop there and ??? again. Thank you.

Com. Domiziano Ratanya: Endelea kumaliza kama hujamaliza kwa sababu ni short.

Lydia Kanda: I can continue. They also said in the national Constitution the new Constitution should be written in all languages for ease understanding.

Also they said on citizenship. The citizenship should be a Kenyan citizen it should be equal so long as the ethnic culture of the applicant must be in Kenya in court. Also they said it was proposed a national trading to be identified and incorporated in the new Constitution.

Land ownership: Both husband and wife to appear in the title deed for family land. Also in case of matrimonial property and also inherited land of the parents.

They said also Children Act to be recognised equally by parents in the new Constitution.

On security the enforcement personnel to be provided with all the necessary facilities and cases where corruption prevails in the enforcement they should be prosecuted by the law.

Women rights and property to be adhered with and strengthened in the new Constitution under review because the parent is poor.

Also the police force or personnel to be managed or empowered by the people down at the sub-locational level in the national Constitution.

In health, health facilities to be provided free by the government of Kenya at the sub locational level and also facilities to be provided at the divisional level by the new Constitution.

Also parents of the abused children to be prosecuted in the national Constitution, human rights policy and principal to be incorporated in the new Constitution.

Personal marriages to be issued with a legal certificate in the national Constitution.

Child labour: Child labour – under 14 years of age to be protected in the new Constitution of Kenya.

In case of orphaned children to be assisted by the government of Kenya through their relatives, schooling and many others.

Provision of disabled institutions to be provided by the government of Kenya in the national Constitutions in all districts and divisions if possible.

Also they said equal distribution of services at the district level to be provided by the government of Kenya in the new Constitution.

Legal authorities to have separate powers from the Central government in the new Constitution.

Magistrates courts: Cases of corruption on exercise of office must be prosecuted and the certificate ?? be cancelled in the new Constitution.

Trust land: Trust land should be demarcated and given portion bits to the residents to enable them develop in the new Constitution.

Equality: $\frac{1}{4}$ government votes for women to be recognised in the new Constitution.

Also academic qualifications for coucellors to be Standard 8 and above in the new Constitution.

Personally laws to be protected in the new Constitution. Also congenital rights to be protected in the new Constitution.

National elections to be voted ballot in the new Constitution.

Enchroachment of rivers and water resources to be avoided. 100 metres away to be protected in the new Constitution for water catchment.

Also freedom of speech and movement to be recognised in the new Constitution countrywide.

Also wife and husband relationship to be protected in the national Constitution.

Rights of property to be protected in the new Constitution and land title deeds to appear both husband and wife.

Gazetted government of Kenya forests to be protected by the community concerned in the new Constitution. Mens succession to inherit land and women succession to be provided for cultivation in the share of their father land in the new Constitution.

Certificate: This is to certify that keeping of records of the proceedings of the Constitution Review in ??? Maendeleo ya Wanawake Organisation – Marakwet district. Thank you.

Com. Domiziano Ratanya: Okey asante sana utanjoja kidogo Lydia nina maswali. Asante sana mama kwa hayo maoni yenu mzuri na mapendekezo yenu ee mlisema kwamba kuna mila fulani zinanyanyasa nyinyi akina mama na mngetaka ziangaliwe katika hio Katiba mpya, Je, ni mila gani ulikuwa labda ukizungumzia?

Lydia Kanda: Okey : vile tumesema hapo, katika utamaduni wetu wa Marakwet, mama anaitwa mtoto, so we want our recognition as women to be seen as people, not as children because in our culture, if somebody comes to my house or home and asks, who is there? Even if I am there, I not supposed to say there is somebody, I say we are here, there is nobody unless there is a man so that I can say there is somebody. That is what we want eradicated as women.

Com. Salome Muigai: I want to ask you my own question but on relying on Commissioner Raiji that you talked about early marriages for girls and that girls should be held responsible for pregnancy without the boys. But now the issues is of governance. What is the role of women, we have talked about local governments, what do you akina mama wanaona wanaweza kuhusishwa aje kwenye uongozi kama wa local government, kama wa parliament, kwa uongozi kwa jumla?

Lydia Kanda: Okey kama vile nilikuwa nimesema wamama wanaonwa kama watoto, pengine mama akiamuka agombee kiti fulani pengine hatakubaliwa kwa sababu hajakuwa na hiyo right ya kuwa mtu mzima. Ingawaje ata saa hii tuna wachache, tungehimiza mama amkie kiti cha parliament ama councillor, community hai-recognise kama ni an adult.

Com. Domiziano Ratanya: Kuna ingine Lydia, siku hizi kuna mazungumzo inaendelea kuhusu kutahirisha wasichana, bado wanaendelea kuzungumza hio maneno katika Kenya. Hapa maoni yako ni nini upande huu wa Marakwet maoni ya Maendeleo ya Wanawake na hata yako pengine mwenyewe?

Lydia Kanda: Okey kwa upande wa Maendeleo ya Wanawake, tunafanya campaign ya kuondoa hio mambo ya female genital mutilation and personally, my views for you ningependa hio campaign iendelee kwa sababu tunaona kuna madhara mengi kwa hiyo kutahirisha wasichana na tunaendelea zaidi, tunatumia wale wamekuwa community elite specially women to eradicate

the culture and to teach may be people in the locality.

Com. Domiziano Ratanya: Okey asante sana nashukuru Lydia, enda hapo ujiandikishe anayefuata ni David Kiptarus na hapo Lydia ametumia masaa yake. Tutumie masaa kama vile nilisema. Tumetumia dakika sita pamoja na maswali yetu.

David Kiptarus: Majina yangu naitwa David Kiptarus. Kuhusu mambo ya hii Katiba, tungetaka nini – nguvu ya rais iondolewe. ??? Kwa upande wa Marakwet hatuna haki ya binadamu. Kwanza tuende upande wa polisi. Nandi ndio hapo iko unyonyaji zaidi ufiada.

Na mambo ya kotini. Iwe independent hakuna kuingiliwa na polisi kwanza huyo court prosecutor, ndio wanaumiza wananchi wa Marakwet. Mtu anashikwa unawekwa rumade hata mwaka moja bila kufanyiwa kwa case. Ambaye ukiangalia upande huo zaidi. Ni hayo tu.

Com. Domiziano Ratanya: Hapo David utangoja kidogo kuna maswali. David asante sana kwa hio maoni ee ulisema kuhusu hii polisi kunyanyasa, mnanyanyaswa kwa njia gani?

David Kiptarus: Kwa upande wa polisi kuhusu upande wa chiefs, unajua kwanza polisi ndio afanye investigations halafu ishikwe mtu sio kushika mtu na kuteswa, na kugongwa gongwa. Kwanza tunalia kama iko mtu wa Nyeri huko kwanzia tunaomba daktari asiletwe pande hii kwa sababu polisi wanaumizanga watu wa pande hii. Hapo ndio mbaya.

Com. Domiziano Ratanya: Asante sana David, kuna swali lingine. Ngoja kidogo.

Com. Salome Muigai: Asante sana Bwana Kiptarus kwa maoni yako mimi nina swali juu ya mamlaka ya rais. Umesema yapunguzwe. Ni mamlaka gani ungetaka yaondolewe kwa rais.

David Kiptarus: Yaondolewe, kama ya rais, hawezi ku-appoint Attorney General. Commissioner ya Police, Commissioner ya Prison, iwachiwe parliament.

Com. Domiziano Ratanya: Okey David asante sana kwa maoni yako umetumia masaa yako vizuri kwa hivyo endelea hapo u-sign register. Tutaenda kwa Susan Kanda ee Susan Kanda ni yule secret--- is it. Susan Kanda tunaye! Susan Kanda pengine hakutaka kuzungumza kwa sababu nimeona, kama hutaki kuzungumza ni kusikiliza ni sawa sawa mama. Magdalene Chebolei.

Magdalene Chebole: Yangu ni chache. Tumefundishwa jana kidogo katika Chepkangei. Magdalene Chebole kutoka

Chebalalia. Sasa nasema kitu kidogo tumefundishwa jana chepkangei, tuseme leo ni mara ya tatu kama imefundishwa sisi. Na yangu kweli tumetumia mwaka ile yote ile Kenya ilipata uhuru mwaka wa 63 na wengine wanasema kubadilishe Katiba. Na kweli tumekubaliana kitu tu ilemini nasema nimestaajabu sana hakuna watu. Sijui watu hawakufurahia kwa nini au ninyi serikali hamkufafanua watu waelewe vizuri hao ni nini kwa maana ni muhimu sana tukipitisha hii maneno na itakuwa mbaya kwa mbele sijui itakuwa namna gani. Sababu mimi nasema hivyo kuna kitu tulipitisha mwaka ingine kama ?? Soko Huru. Tulikubaliana Soko Huru tukakubaliana, tukapiga makofi, tukafurahi baadaye tukalia kimoyo moyo ikakuwa taabu sana. Kwa hivyo wananchi wote, wamama wazee tuangalie sana mambo ya Soko Huru na viongozi wote katika jamii hii yetu ndio tusije tukalie nyumae. Twaangalie vizuri sana.

Maoni yangu ningependa asikuwe leo peke yake ifundishwe, ifundishwe sisi tena mpaka tuelewe mambo ya Katiba. Kwa maana saa zingine watu wengine:ingawa kweli watu wote hawezi kuja kutoka nyumbani tutaangalia tu vile tutafanya.

Naenda ya tatu sasa; mimi naona upande wa serikali ilifurahia hio ujama ingawa sijui alikuja mahali ingine lakini ni maoni yake. Kitu ile nimeona katika centre hii bado yule rais ya polisi awe office tu yeyote. Ukienda hapa nikipoteza mbuzi yangu au ng'ombe yangu nakienda Chiefs' office unaambiwa ulipe pesa ya askari, na mimi ni mkulima mdogo kama mimi, nitapata watu pesa ya kupeleka hao askari mpaka kortini. Usipokuwa na pesa hutafanyiwa hio kesi yako.

Ya nne halafu nimalize, kuna shinda fulani hii Marakwet kwetu District vile nyinyi mlisikia ata kila mtu kama Mkenya alisikia. Ukijenga mahali kama kapsoit, kama Harur au wapi iwe kama police station, hakuna kitu ile polisi yenu anasaidia sisi. Kwa maana ikiambiwa imepeleka ngombe kiasi fulani hapa, au kondoo au punda, anaambia wananchi wenyewe, mtangulie, mfuata mali zenu. Hatutaki. Anasaidia sisi nini? Sasa wananchi wenyewe ana mkono mtupu na hawa anatii serikali vile inatakikana, na ni watoto wetu, na wanataka watuachilie?? Kenya hii. Asante.

Com. Dominiziano Ratanya: Haya, asante Magdalene. Akindikisha hapo jina lako.Twaendelea kwa mwingine Gideon K Yego, Gideon Yego ni wakati wako sasa, Yego hayuko? Okey kama Gideon hayuo twende kwa Paul Kipsang. Paul Kipsang, Yuko William Cheboi. William ni wakati wako.

William Cheboi: Mimi naitwa William Kipatarus Cheboi natoa shukrani kwa nyinyi kuwa hapa kuja kusikia maoni ya Wamarakwet. Sasa mimi nitaanza kwa mambo ya mashamba. Hapa kwetu kuna mashamba aina mbili. Ile ya wenyewe kutoka zamani ambayo iliwekwa mpaka na mababu zetu na hiyo ninaonelea si mzuri watu kung'ang'ania kwa watu wengine na kuondoa jamii fulani kama ni watu wachache wengine wale wamepata nguvu wanaingia na kuhamisha wale wengine na wao wanaendelea na kufanya kesi na kusema ni yao. Hio sheria ningetaka ikomeshwe kwa kuachia machief wafanye kesi ya shamba. Sio mtu kuingia mpaka kwa kortini kwa maana yeye ako na uwezo na kufukuza mwingine kwa shamba lake na kortini wanaamuru hii shamba ni ya mtu fulani kwa maana yule mtu mwingine iko pressure ya kutosha. Hio sheria ningenelea iwashie wazee na ma chief wawe wakiamua kwa maneno ya mashamba.

Na ile ingine ya pili kuhusu shamba ni yule mtu ambaye alinunua shamba lake tuseme wale wazee wa zamani walipata kutoka kwa wazungu na walipata shamba kubwa kubwa. Unakuta mwingine ako na ekari elfu tatu au zaidi na ingine sasa inakaa kama forest, wanyama inaishi, na wakenya wote hawana mashamba ningeonelea ni vizuri huo mtu, serikali aone kama yeye haja develop hizo mashamba au shamba hio hizo sehemu zingine zimeashwa kama forest auze. Nakupee wananchi. Kwa maana sio mzuri kufuga wanyama kwa shamba na wengine hawana mashamba.

Twende kwa mambo ya natural resources kama forest, hapa kwetu tuko na forest kubwa katika Marakwet. Na kwa zamani, forest ilikuwa imewachiwa wananchi wenyewe wawe wakichunga. Na ililindwa mzuri sana mpaka sasa hii sheria ya kuja ya kusema forest yote imepeanwa kwa wale walinda forest na yetu ilikuwa imelindwa ndio unaona kwamba Marakwet bado wako na forest yao. Na kama ningelijua wa Marakwet wako na forest ya kila clan, inajulikana ni ya fulani na hawajaharibu forest tangu zamani. Walikuwa wakienda huko na kutoa asali yao na kuchunga kama mtu mwingine angekuja kufunga mchinga yake ya asali kwa forest ya mtu mwingine. Walikuwa na right ya kuuliza ni ya nani hii mzinga, wanatoa huyo mtu nakumwambia kwenda kwa forest yako. Ndio forest yetu tulilinda hivyo mpaka sasa.

Na twende kwa upande wa elimu: Elimu kweli tuna watu wamesoma. Na ukikuta wameachwa nje. ??? unaweza kuta mtu hana elimu ako kwa kazi. Hio si Kenya ya sasa? Hiyo mambo ingekuwa iliisha zamani wakati wa kikoloni. Sasa ndio tunazomesha watoto ili wachukue nafasi kwa wale watu ambao hawana masomo sana sana. Hiyo serikali ingechunguza sawasawa. Ikifika wakati wa kuajili watu kazi waajiri kulingana na masomo ya mtu sio kwa kupendelea, kwa kuona huyu ni rafiki, huyu ni ukoo fulani, hapana.

Haya tukuje kwa mambo ya security. Katika security, kwa kweli kuna watu wameajiriwa kulinda amani na tulikuja kusikia hivi majuzi sisi tulikuwa na matata matata na sisi wenzetu hata sasa haijaisha, hawa wapokot. Na kusudi ya hio vita kuanza kuna silaha zilipeanwa na serikali ya kulinda; hii inaitwa homeguard weapon. Home guard weapon sisi tutapiga nani – tuko katikati ya nchi na hatungeona maana ya hiyo, kuleta silaha na kusema Wapokot wajilinde. Hio ni kumwambia kama ukoo wa nafuu. Ukiwa na watoto kama watatu, na mwingine amepiga mwingine, unampa yule fimbo na kumwambia ujilinde; hio ni njia ya kumuniiza yule mtoto, watapigana mpaka mwingine auwawe. Na tungetake hiyo silaha ambaye ilipeanwa na serikali ambaye niyakulinda nchi tuwachie wananchi ambao wameajiriwa walinde, nchi walinde. Hio silaha haina maana kwa maana sisi tuko katikati ya nchi na hatuna maana na hiyo. Tuseme kwamba tunajirinda wenyewe na askari watafanya nini? Hii clashes ilianza hapo. Na watu wengine wakanunua yao wale ambao hawakupata uwezo, hawakupewa ndio wakajitafutia. Walikuwa wamenyanyaswa na wale wengine.

Haya ya mwisho, tuje kwa upande wa mshemiwa raisi. Kwa kweli mamlaka alipewa na mamlaka hiyo ambayo rais alipewa si mbaya lakini tumefika wakati ambao sisi wananchi tumeanza kulalamika kwa yeye kuteuwa watu ambao hata hawana elimu na kusema mtu aanze kazi mara moja kwa maana hana watu ambao wanasema na yeye au wanaketi kamati ya kusema fulani

tumebadilisha na fulani.

Ee, tukuje hapa wakati wa kuchagua mawaziri na manaibu ya mawaziri. Tunakuta ni yeye peke yake anaamua tu na kusema fulani aingie ofisi fulani mara moja. Wangekuwa na kamati ya kukaa pamoja na kuona nani iko na elimu tuchukue kwa upande wa Ministry of Education ile mtu ambaye iko na elimu ndio angeongoza kuliko ??

Com. Riunga Raiji: Jaribu kumaliza hapo

William Cheboi: Kwa hivyo hio uwezo ya rais ya kusema huyu mtu ameanza kazi mara moja ibadilishwe na watu watakaa na kujua nina hata fit kwa sehemu fulani. Asanteni sana.

Com. Riunga Raiji: Okey twende kwa mwingine. Bwana william nenda pale u-sign register yetu. Kuna Joseph Ndiwa – Joseph Ndiwa ni wakati wako, okey naona Joseph ulikuwa unataka kuzikiliza. Asante sana Joseph. Kwa hivyo tutaenda kwa David Chelimo, hata yeye anataka kusikiliza tu, Cecilia Chepkok, Daniel Kilimo, Okey utasema jina yako mzuri ili inazwe kwa machine yetu.

Daniel Kerima Kibiatich: Commissioners na wageni walioko na sisi mimi naitwa, Reverend Daniel Kerima Kibiatich na kwa Katiba mpya, uhuru wa kuabudu uendelee, watu kuabudu mungu bila kizuizi chochote.

Jambo la pili ??? (inaudible start of tape)

The main gender equality, wamama kuwa sawa na wazee, uwezo wa mzee nyumbani katika Katiba iendelee kudumu. Tujifunze kichwa ya nyumbani. Unajua hii kelele yenu ya equality, hii inaweza kufuja kichwa ya nyumbani mpaka maana anatoka nyumbani, anapasuka kwa hivyo hii Katiba mpya iendelee kichwa ya nyumbani bado ni mume. Fullstop. Usisahau hiyo.

Jambo lingine tutumie tena rasilmali yetu kama Marakwet kwa njia nzuri. Mambo ya corruption serikali iwe katika Katiba ichungie wananchi mali yao ili mtu moja asikule yote, tukule pamoja resources ambayo tuko nayo. Mambo ya kuhonga ikwishe. Ikiwa unauza mahindi ufanye nini! Hata polisi wakomeshe hii kazi ya kupewa chai kwa hii Katiba mpya, ya barabara, ya wapi, kortini, tusime hiyo ili tusifanyie watu kazi ya kuhongana.

Inginge hata serikali yetu ituongezee mshahara kwa Katiba mpya ili wasiwe na tamaa ya kupewa kitu.

Inginge askari yetu tupewe ruhusa ya kuishi na bibi zao katika kambi. Ukimwi inazidi kwa sababu hakuna bibi kwa kambi ya askari. Mimi nataka askari aende na mke wake kazini kwa hii Katiba mpya. Sijui itakaa aje, tutachunguza tu, hii ni maoni yangu akae na bibi yake kambi.

Wale walemavu watunzwe katika Katiba mpya. Watunzwe katika Katiba mpya. Na shule ithaminiwe na makanisa, katika Katiba mya kwa historia, mashule mengi ilianzishwa na makanisa na si mzuri kutupa kanisa nje ; wao wathamini na utamaduni hi mzuri za kanisa zidumu katika mashule.

Na kama vile mtu alisema, wananchi wamiliki forest, iwe ya wananchi na clan ya watu kwa sababu ikiwa tu ya walimwengu au serikali mambo inaweza kuharibika. Asante hiyo ilikuwa maoni yangu tu.

Com. Domiziano Ratanya: Okey. Asante sana Daniel, utaenda pale uandikishe kwa register yetu. Asante kwa maoni yako. Sasa twende kwa Father Samuel Kigen, Father Samuel Kigen uko wapi? Sasa Father ni wakati wako.

Father Samuel Kigen: The commissioners na watu wengine, asante sana tuekutana siku ya leo ili kujadiliane juu ya Katiba yetu. Na vile mama mwingine alisema kwamba alishtuka ; Father Samuel Kigen, Jina ni Father Samuel Kigen; vile mama mwingine alishtuka ya kwamba kwa nini watu si wengi, najua Marakwet watu ni wengi, sijui kulikuwa na communication breakdown.

Mimi niliona kwa newspaper sijui kama waliweka kwa redio, waliweka, then, asante sana. ??? so ya pili ni juu ya civic education. I don't think the Civic Education was well done at the grassroot, not very. I don't know whether you had a group, we had our group at the church. We never met with people from ???. So what we are presenting now is not very strong as such because the civic education at the grassroot was not done well. If people got it it was just a mere chance but most of the people they never got it.

Ya pili let people know their Constitution. Let people know their constitution. Translate constitution especially this being a new constitution, let us translate it into Kiswahili. Let us teach it in our school. Otherwise to make it like a private thing for MPs, No. Let us make a constitution to be owned by the people of Kenya. It is our constitution and we are the ones to know it.

The third one is: How to deal with corruption. The new constitution should bring out clearly how we should bring corruption cases and economic sabotage. They should be prosecuted not to be left scot free. I think it should be a criminal offence to steal peoples money na unatembea tu. So I think the new constitution should defend the poor and not the poor dying through the hands of the rich. So I think the new Constitution should belong to the poor ??? is not doing that at all.

Another one is the constitution to ????? should be entailed in the constitution. I don't know if it is. If the president today decides that we should not continue with the constitution, I don't think it will continue at all. I don't know. May be you may answer me that. People want a constitution where if the president decide people can say no. The way we have given out our good points we expect that these points should continue, until it goes to the constitution. Nobody should try to derail the constitution process. You know what is happening now is an idea of election- and constitution. It should not affect our points.

All equal share in the whole of Kenya in the idea of resources. We should share the Kenyan resources equally. In rural places unlike in urban centres we should share our resources equally. In Marakwet, we don't have a tarmac but I think we are Kenyans. We are supposed to share our national cake equally. The president of the day should take the government resources to his place should share equally, so I think that it should be entailed in the constitution.

Also freedom of worship should continue but I think it should be trimmed a bit. Because the moment somebody can start a church and mislead people. So in Kenya what might come up very soon is what happened in Uganda – the Kinungu case, if we don't try to, let us not ??? freedom of worship. Everybody can start a church. No. It should be trimmed and checked the genuineness of the person starting the church. Thank you very much. God bless.

Com. Riunga Raiji: Father Samuel just wait.

Com. Salome Muigai: Father Samuel I have one question or clarification one that the Catholic church were major partners at the national level in teaching education. We do appreciate that it has not gone as well as it could, but that partnership was there and it was agreed because we agreed that the Catholic action tayari wako mashinani na wamesaidia pahali pengine wamefanya kazi nzuri sana pahali wangeweza kama tulikuwa Arol jana na kanisa ilifanya kazi nzuri sana kuwafundisha wananchi na kuwatayarisha kwenye huu mpango na tunashukuru pia kwa ajili ya hio. Mimi nina swali kwako na swali yenyewe ni juu ya kusema kuwa Katiba mpya inatakiwa ku-protect the poor. Can you give us some of the ways that; suggestions yenye tungetumia kuhakikisha hii Katiba mpya inajari maslali ya walio maskini. The first one is about education. Education especially the primary education. I think it should be free, if we give free education we shall be helping the poor. That is what I said the sharing of the cake and removing the idea of corruption at all because corruption usually it goes down to the poor. It is the poor who suffers. If somebody steals 1 billion shillings he does not dance with the local man (inaudible – laughter)

Com. Riunga Raiji: Ee peleka hapo na u-sign register yetu. Tutaenda kwa Patrick Chebelion. Patrick Chebelion.

Patrick Chebeliel: Ee asante sana macommissioners na wamarakwet wote. Hii ni wakati mwingine kubwa sana katika Kenya yetu kama Wanakenya.

Com. Riunga Raiji: Sema jina yako inaswe kwa machine yetu.

Patrick Chebeliel: “Patrick Chebeliel ’ Jina yangu ni Patrick Chebeliel, basi nilianza kusema ya kwamba leo ni siku kubwa katika historia ya nchi yetu kwa sababu tunajaribu kurekebisha Katiba tangu enzi zile za ukoloni na Katiba ilikuwa imefanya mataabiko kwa mara mingi. Kwa hivyo nafikiri leo wanafanya overhauling of the Kenyan Constitution ile kitu inaguzi maisha ya watu sana ni security. Katika Marakwet, tumekuwa na insecurity kwa muda mrefu kama bile mtu alisema ya kwamba

wakati wenzetu wale Wapokot walipata nafasi ya kupata mabunduk ndio insecurity katika sehemu za valley iliharibika sana. Kwa hivyo tunasema katiba mpya ihakikishie watu wetu ata Wamarakwet ya kwamba security ni paramount sababu hata kazi yote tungefanyia developmenet katika miaka ishirini iliyopita, ilikuwa niku-prevent security huko.

Sasa tuko kwa District Commissioner ya treasury, imeenda huko chini inaenda huko chini badala ya sisi kufanya kazi. Kwa hivyo sisi kama Wamarakwet hatujaendelea hata kidogo. Kwa sababu pesa ote, ile allocation yetu inatumika kwa security. Basi kwa hivyo ningeliza hii Katiba mpya ihakikishie sisi ya kwamba security iwe ya maana sana pengine wale watu wakuishi huku, serikali imechukua responsibility kwa ??? building schools – boarding schools on those areas and may be police station in those areas. Lakini ya maana sana is civilisation – education. Educate them because they are primitive .

Kitu kingine ni ya kwamba natural resources zetu watu wanataja – mini niko na maoni kidogo kwa forest tukiimba kwa kila clan, saa hii kuna massive destruction, na tukiwachia clan, unajua saa hii ndugu yangu anafieka huko, anaendelea kuharibu na kuharibu kwa hivyo serikali wangesaidiana na clan, mine is to put a different appeal, wote tusaaidiane. Tukiacha clan, haitakuwa effective sana.

Land issues kama vile tuna sehemu kidogo hapa hchini ambayo bado kuwa demarcated. We are asking the government to demarcate all our land so that we have a tittle deed. Kweli tuko na communal land today kama kitu ikipatikana kama minerals na oils na kadhalika, serikali wanaingia huko kudai ownership, so we want the demarcation.

Na communal land hata kitu gani kipatikane, lazima the community ama watu wa clan hio waulizwe, wapate kitu hiyo. Na hatutaki ujaja ya construction ya zamani ya kusema kwamba kitu ikipatikana kwa shamba yako, yako ni futi sita na ingine ya chini ni ya serikali. Hio ni abunwasi. Hiyo ni mbaya. So we own the ground upto a thousand, or a hundred feet na huko juu, pia hata huko juu, we have rights; kama hiyo ni kuokota shamba yako, we have rights to a certain height in the sky because you can build a house and all that.

Inginge commissioners ni ya kwamba majimboism – majimbo ni njia moja ya kufanya decentralisation of natural resources. Kwa wakati huu pesa ikipatikana, pesa napelekwa Nairobi, kila kitu Nairobi, so tunganasema ya kwamba majimbo iweko lakini watu wote wawe free kufanya biashara mahali popote lakini there has to be decentralisation of resources. Hio sio kusema ati watu wanatawanyatawanya sana kama nchi zingine kama Nigeria. They have federal system of government, nchi ingine kama Germany, they have a ??? system . Kwa hivyo why not us? Majimbo ni kuhakikisha decentralisation of resources.

Appointment of commissioners ni ya kwamba people like President should not indulbe themselves in appointments. Tuko na Public Service Commission na hii Public Service Commission walete mtu moja kwa kila district representing sababu katika hii parastatal yetu leo unaona district zingine wako na watu karibu ishirini while hapa Marakwet we don't even have a head Managing Director, hata mmoja. Wengine wako na 50. Kwa nini tuwe just one representative kwenda Public Service

Commission na President to desist from this appointment in the new Constitution.

Ingene Bwana Commissioners maneno mingi inatokea katika Kenya Gazette. Kenya Gazette, appointments, nini, mambo mengi, now how do we get this Kenya Gazette? Is it available? Wewe unaweza kustakiwa na inasemekana ilikuwa kwa Kenya Gazette, Kenya Gazette inaletwa kwa DC, pengine County council, lakini mahali pengine hapatikani. So, can this Kenya Gazette be made available in the new Constitution to wananchi . Let it be sold like other periodicals or other dailies, yaani Standard, Nation na kadhalika.

Com. Riunga Raiji: Ee Chebeliel wakati wako umekwisha, just have a minute to wide up.

Patrick Chebeliel: Kuna kitu moja ambaye mama moja alitaja ee wananchi ni ya kwamba kama mtu akiuwa mwingine hapa Marakwet, watu wa hiyo clan ambayo mtu huyu anauwawa inafanya nini? Inafamia, sasa wanafamia yule mtu ambaye ameendelea katika hiyo jamii. So can the new Constitution kusema ya kwamba kama fulani ameuwa fulani, wacha huyu a face the consequences not te community or the brothers or the relatives. Eee is that not true?

Kwa hivyo tumeona mama hapa na nguosafi. Nafikiri Kenya should have also a national dress. National dress, mtu, akionekana huko, Nigeria, Uganda, anaonekana ni wa Kenya. So we can have a nationa dress especially women. Lakini men, waendeleo na tai zao na kadhalika. (laughter).

Kwa hayo machache mimi nasema thank you very much.

Com. Riunga Raiji: Okey. Ngoja kidogo. Pengine tuna maswali.

Com. Salome Muigai: Asante sana Bwana Chebeliel kwa maoni yako. Mimi ningetaka kuuliza maswali mbili au matatu ya ufafanusi. Ya kwanza ni hii demarcation of land. Unataka lands ikuwe demarcated ipatiwe nani? Yaani tittle deed itakuwa na jina la nani? Hio ni swali langu la kwanza. Nina maswali mawili ama matatu hivi.

Pia umesema kuwa ungetaka kuona clan na serikali ikishirikiana kuangalia forest. Hii tungetaka utueleze concretely the attitudes that you have in mind because the clearer the submissions you give us, the easy it is for us to be able to see how the Marakwets will see this issue. So the issue of land is something that I would like you to review it.

Last but not least, why should women have a national dress when the men are tying ties?

Patrick Chebeliel: Thank you very much. Madam Commissioner, demarcation ambayo ninasema watu lazima wapewe ee legal anarchy – individuals –

Com. Salome Muigai: Ah, so, can you make it very clear what the role of the clan is, what the role of the government is and what the role of individuals in the ownership or in the stewardship of the land in this area.

Patrick Chebeliel: Right. In some parts of Marakwet, we have communal land and everybody knows they used to demarcate using stones. So take for example myself, I have two sons and three daughters. Maybe the government will come, surveyor will come and say ; okey give Kiplagat that one. Give Kiptoo that one and so forth, so that is what we mean. We mean let the government come and survey and give us the relevant documents. Agricultural forests I have a nimeona ya kwamba kama ikiachiwa tu raia, destruction will go ahead because you don't want – huwezi under kushtaki ndugu yako, huwezi kwenda kushtaki dada yako na kadhalika kwa hivyo the government should chip in ku-protect pamoja na wananchi.

Now, I feel kama wanaume tuliambiwa tufae ile ya Ki-nigeria na kitu namna hii na kubeba, may be the tie, we have identical tie, imeandikwa Kenya, lakini akina mama wa dress kama wewe. Thank you.

Com. Riunga Raiji: Okey Bwana Chebeliel. Mwingine hapa ni Abdi K Kipchoge. Abi K Kipchoge, endelea.

Abdi Kipkemboi Choge: Asante sana Commissioners pamoja na wananchi ambayo wameweza kutulia siku ya leo. Yangu tu macommissioners ambaye ningesema hapa mbele yenu – Abdi Kipkemboi Choge. Ningetaka kusema katika Katiba pia ya kwamba serikali pia itawaliwe na serikali za wilaya. Sababy yakusema hivyo ningependa kusema ya kwamba pesa yetu hutoka Treasury na anakuja kutawaliwa na District Commissioner. District Commissioners ni mtu foreign anaweza kutumia pesa kwa njia mbaya na ningependa pesa hizo ilundishwe kwa Chairman wa County Council kwa sababy Chairman wa County Council ni mwananchi wenyewe wanamchagua. So atachunga hiyo pesa kwa njia inayofaa kwa sababu atajua yeye ni electorate.

Inginge tena, hii mambo ya councillors, madiwani ni mzuri kuwa na elimu yao ya kila siku pamoja na ile interview yao ya kufanyiwa ya lugha, hiyo inatosha. Sababu ni watu waaminifu na ni watu wakuwakilisha mambo ya wilaya sababu tuna wazee wengin ambao wangependa kufaa kofia na ikisemekana elimu ya juu zaidi, hio watu hawatakuweko. Kuna wazee karibu rika mne ambayo wako sasa, kuna ingine ambayo inaitwa Kagero, Chumo, Kaberechiko, na ni watu waaminifu lakini kama mtu anaweza kufika kiwango fulani hawataambia jamii ukweli.

Inginge tena, mimi ningependa serikali katika hii Katiba mpya, Serikali iluhusiwe hii serikali ya wilaya zaidi. Chief achaguliwe na wananchi na manaibu wao sababu chief ukifuatana na yeye anaweza hata kukunyang'anya wewe bibi yako na anakaa mpaka retirement. Kwa hivyo mzuri chief achaguliwe. Kwa hivyo akifanya kosa, atajua baada ya miaka mitano, ataondolewa. Kwa hivyo atachunga kazi yake vilivyo.

Inginge tena Bwana Commissioners Wamarakwet wametaabika sana na vita a hii majirani yao Wapokot. Mimi ningependa kusema, serikali ilitoa ilani ya kwamba mtu asiwe na ng'aling'ali lazima mwananchi analindwa pamoja na mali yake, na mimi

nashangaa juzi, majirani zetu wa Pokot walikuja na wakawaumiza Wamarakwet wakachukua mali, wakauwa watu kwa bunduki na wakaiba ng'ombe ambaye ukienda kutoa kifungu yao, saa mbili unaweza kuhukumiwa kifo. Na hakuna hatua yeyote ambaye ilichukuliwa. So, mimi ningesema, ukikuja kupiga report, kueleza ya kwamba vita kama hiyo imetokea kule chini, OCPD – hii watu wa security wanaanza kutumia delaying tactics. Anakaa, kama una report saa moja, wanakaa mpaka saa saba ndio wakuje. Wanajifanya sawasawa wanafanya kazi katika wanaenda huko, wanamangamanga huko na anajua tu, hao watu washatoka – immenda.

Ee, Chairman ya County Council ipewe uwezo zaidi kwa sababu nchi ni yake. Wa control hapa hii security kwa sababu wanajua ni mara moja na wakizinzia, anakasa wao waende mara moja kutatua hiyo shinda.

Basi mimi nafikiri yangu nimefikia hapo mheshimiwa.

Com. Riunga Raiji: Okey, asante sana Bwana Abdi . Nenda hapo kwa register yetu. Kuna William Kipyegon.

William Kipyegon: Kwa majina, naitwa William Kipyegon nikianza kutoa maoni yangu ya kwanza ni juu ya land ownership. I want a Constitution whereby every Kenyan is restricted to have a maximum of 1000 acres. If you have more than 1 000 you surrender to the government so that certificate of land may be given. This will also check mambo ya land grabbing because in Kenya today, the rights of the politicians somebody's even have more than 10 000 acres and still wants another land. So when we have a Costitution every Kenyan will have land.

Another one Local Authorities: I think these people should be empowered and should be made autonomous to set up their own parliament whereby all the resources alloted to that district to be managed by the local authority. I think this one help much to check on the distribution of the natural resource like here in Marakwet, I am sure the Commissioners yo are expecting to have a tarmac road in Marakwet. It is very unfortunate that mtapitia fumbi. If we would have a national fund directly located to Marakwets, I am sure we would have some kilometres of tarmac road. So if the resources are divided at the national level. Then the Marakwets will have their share and set their own priority under the County Council.

There is also this issue of government insecurity. To me, I am seeing that the government should compensate for those people who have been affected by insecurity like Marakwets. The other year so many people were killed and they were not compensated. Since it is the work of the government to protect its citizens, and if it's the work of the government to protect its citizens, we should have that obligation to compensate those people who have been killed by bandits.

Another one is medical health care: Medical Health Care should be free for all Kenyans in the new Constituency. Why? Because when we have healthy people we shall have a health nation. Without health people, there will be nothing which is happening in that country. So the government should provide medical care, health care for all free so that every other organ of

the government will run well. When we have a sick person, everything else will be paralysed.

There is this case of gender. To me the question of women of equality of women to men should not arise. Men and women have got their roles in society a woman has got her own role, so I don't see why a woman should be equal to man. Even in the bible a man is the head of the house hold. So where does the situation whereby these people can be equal because in homes there will be a lot of family instability. So the man should be the overall boss in the home. In other areas like education and other things, yes, they can be equal, there's no objection and when it comes to the management of the family, the man should be the boss.

There is this case of presidential powers. I think this has been the most abused in our country whereby even somebody who is not able to hold that office is given a post to run and that why in Kenya we are ranked amongst the most corrupt in the world. Why? You give somebody a post who does not know what to do. So public posts like chief appointments should be voted by parliament so that if you mess you will be dealt as per the law. But this idea of having a cousin, a brother, a clansman holding office should stop if Kenya will go away from this trend of corruption.

Com. Riunga Raiji: William jaribu kumaliza wakati wako umekwisha.

William Kipyegon: There is a case whereby somebody holds a public office and is charged on corruption – then you hear, tomorrow he is the head of another parastatal. I think that one should stop. If somebody has been charged on corruption, he should be declared unfit to hold any other public office. Thank you very much.

Com. Riunga Raiji: Njoja kidogo William.

Com. Salome Muigai: Thank you very much William. There's a question from your views. A question or a clarification. You have said that “serikali inatakikana kufanya compensation kwani kazi yake kulind watu na mali yao” Ungependa compensation ya aina gani? Hilo ni swali la kwanza.

Swali la pili umesema juu ya “equality does not arise because people have different roles, wewe unawza kuwa mwalimu na mimi nikawa daktari, sisi tunafanya kazi tofauti, does that stop us from being equal even though we are playing different roles because we are both giving our contribution towards the development of the country or our home. So the equality does not sound as we feel it is part of the acting under which we are operating. It is not a question of people doing equal roles. It is a question of giving equal value to values of people doing different work. And I think that also it is the same thing we've been telling us. We have been saying that the Marakwets, the Kikuyu and everybody should be equal, even though they are different. So we are looking for ways of sending this equality in differentiation within not just the working mates but at home. So I am looking for your thoughts on this as well.

William Kipyegon: On roles, when it comes to employment and any other part of life, me, equality it can be there but at the family level whereby a mother is supposed to perform certain functions, a father certain functions at the home level. You hear of these issues like when you are married and you are asked to take care of the kitchen today. That is the area whereby I am saying it should not arise because at the on-stage level, the man should be the chairman of what is happening around the homestead.

When it comes to public life yes we can be equal outside there. But at the home management, it remains on the man.

And the security compensation – like now 3 years ago, we were carrying but some immunization on polio, some children were killed in parts of Marakwet district and the government never compensated that loss. Since there is a government policy that all children are to be immunised so that's the area where I am saying the families affected should be compensated that loss. If a man is killed by Pokot or a Pokot is killed by a Marakwet, that homestead should be compensated because the loss of that man will have some adverse effect on that family.

Com. Riunga Raiji: Okey, asante William ee, kwa sababu sasa naonawatu wemekuwa wengi, tulipoanza walikuwa wachache, na ningependa kuwakumbusha vile tulikubaliana hapo tulipoanza ili wale hamkuwa sas wajue. Kitu cha muhimu nikwamba tulisema lugha, unaweza kuongea Kiingereza ama Kiswahili na hata lugha ya kienyeji: ya hapa mnaita kimarakwet ama lugha yenu local munaitaje? (Jibu – Marakwesh). Kwa hivyo uko free kutafuta mtu wa kutujulisha vile unasema. Naona watu wengi hawataki kusema pengine kama ni mambo ya lugha, kuja useme kwa lugha yako, upeane maoni yako ambayo itasaidia kubadilisha Katiba yetu. Hio nilisema na uwe free. Hapo nilisema kwamba uko huru kupeana maoni yako kwa Tume hili ya Kurekebisha Katiba ya Kenya. Usiogope yeyote. Usiseme ya kwamba ati Bwana yako atakupiga njioni ukienda kama ukisema maoni yako ama bwana aseme atapigwa na bibi yake ama mambo zingine. Kwa hivyo usiogope. Hapo nilisema hapo mwanzoni. 2, 3 kupeana maoni yetu ili tubadilishe hii Katiba yetu.

Nilisema hapa ya kwamba time, yaani wakati ambao napeana hapa tulikubaliana hapa na wale tulipoanza na wanaendelea mzuri, mpaka sasa hakuna mtu nime-penalise mambo ya masaa lakini wale wamekuja sasa ningependa kuwakumbusha kwamba ukiwa na memorandum, memorandum inaweza wakati mwingine kuwa kubwa kama hii, hutakuja hapa kusoma hio memorandum, ni kupeana yale ya muhimu tu – points, points na halafu memorandum tunaitaji sana, uweke pale, tutaikagua, itaangaliwa, tuna hawa watu wakufanya hiyo kazi na hapo nitakupatia dakika tano kwa kupeana maoni yako. Ukiwa na memorandum ambayo utapeana machache, dakika tano, ukiwa huna memorandum ni kuzungumza tu kwa mdomo, dakika hiyo tano. Si zaidi ya dakika tano lakini unaweza kuongea dakika chache lakini si zaidi ya tano, ili watu hawa wote wakati tunamaliza, tukifikia njioni ama wakati fulani, kila mtu amesema kitu . au mnataka wengine waende bila kusema kitu? Yule yeyote anataka, lazima apatiwe nafasi. Lakini kuchukua nafasi yote pengine wengine wataachwa. Kwa hivyo tukubaliane hivyo na msipitishaye hayo.

Lakini unaweza kuwa na memorandum na useme wewe hutaki kuzungumza uende pale kwa officers wetu, upeane

memorandum, uweke signature na uketi hapo usikilize vile wengine wanasikiliza ama ukitaka kwenda uende. Uko huru.

Kuna pengine wengine hawataki kusema jambo lolote hapa. Hata, hivyo, wakae tu, wasikilize wengine, mtu akibadilisha maoni yake aseme tu, asubuhi nilikuwa nimesema sitasema lakini sasa nimewekwa bidii nitasema, tutakukubalia. Hakuna taabu. Kwa hivyo tuendeleo na list yetu. Yule ambaye anafuata William Kedago, ni Selina Kedago. Selina unaongea, pengine unapeana memorandum. Its okey. Selina, nilisema kama ukiwa na memorandum, you can highlight for 5 minutes lakini ni wewe vile unataka ni sawa sawa. Okey, Selina ametupatia memorandum na hapo ni sawa sawa. Twende kwa Gabriel Chemweno. Na ukija hapa twambie jina lako ili hii machine ichukue jina lako.

Councillor Gabriel R Chemweno: Kwa majina, mimi ni Councillor Chemweno, Gabriel R Chemweno – Vice Chairman ya KANU Marakwet district. Basi kwa nafasi hii ndogo, asante commissioners kwa kufika sehemu zetu ya Marakwet. Yangu tu ningetaka kuongea sana kuhusu freedom ya kila mtu ama uhuru kwa mtu kutembea na kuwa huru kufika sehemu zetu hii, ya mashambani, ama wilayani yetu ya Marakwet. Langu tu, ni ngetaka kuongea sana kuhusu freedom ya kila mtu; ama huru kwa mtu kutembea na kuwa huru kwa sababu wakati mwingine, unaweza kupita pahali na unapata askari ambaye ako kwa kazi yake, halafu anaanza kukuliza ulikuwa unaenda wapi, wewe unajua sisi ni polisi? Wewe unajua sisi ni hii? Mpaka mtu anaaza kuwa na woga, kwa jambo ambaye hakutarajia iko mbele yake. Kwa hivyo, jambo kama hilo, iwekwe sheria, ya kulinda mtu yeyote. Kama una nyanyaswa, unapiga repoti. Askari kama huyo anastakiwa, na kufutwa kazi, na alipe yule damage. Kwa sababu ameharibu yeye. Amemweka woga kwa njia yake.

La pili, tumekuja hapa mbele Bwana Commissioner kwa sababu nchi yetu Kenya ni mgonjwa. Kwa sababu gani nina sema Kenya ni mgonjwa? Ni kwa sababu ya corruption. Ndio inafanya sisi mpaka tunarudi kusema pengine sheria tuli tunga vibaya, pengine nini ilienda vibaya. Sheria moja itungwe, kama mtu anafanya corruption, anatolewa, pahali ya kazi, public offices, atoke nje. Hapana transfer, kwenda kuharibu pahali pengine. Sheria kama hio itupwe. Na tena, arudishe ile mali ameiba si kutolewa tu na kuacha aende na mali. Mimi nalaumu sheria ya zamani kidogo kwa sababu waliweka umuhimu, mtu akiiba sindano, anafungwa miaka mingi, na mtu akiiba pesa mingi, anawachiliwa kotini bure. Mwenye alikuwa anatamani kuiba sindano, ni raia yule maskini, ambaye anaona sindano ni kubwa, na yeye ameenda kufungwa. Basi, sheria kama hio iondolewe, na mwenye amechukuwa vitu, ya wananchi inafuatwa na arudishe hio pesa; sio transfer.

Kuna ugonjwa ingine. Sheria tena inaweza kuwa sumu, kwa wale wanatumia vibaya. Unaona wakati huu polisi wamekuwa Bwana wa mabwana wakati huu. Kwanza mimi ni Councillor sasa, na sina huru kwa ile ofisi yangu ya OCPD yule yuko huko. Nikienda huko, kwanza wananiambia wewe unaitwa nani? Unataka nini, ilete hapa! Ananisumbua kabisa mpaka ninaona kuna kitu ninaweza sema, ama nikikosa karatasi moja, nitawekwa ndani. Kwa hivyo mimi nataka mtu awe free; kila mtu aseme mambo yake, kama ni uongo, waseme, na baadaye athibitisho, ikikosa, niwekwe ndani. Na binadamu, sijui aliumbwa namna gani. Kuna mtindo moja iliingia mwili wa binadamu. Anapenda hata kusema wacha naenda kuharibia mtu fulani jina. Anaenda anasema ameiba hii, na yeye hajaona. Kutungwe sheria ya kuharibu mambo hii. Mut akiniharibia jina, baada yangu kushinda kesi, kuwe na fine ile anatakiwa kulipa, na isiwe chini ya elfu mia tano mpaka milioni moja. Haya, nimemaliza hio.

Ingingine ni juu ya timu inasimamia wilaya inaitwa Security team. Ile ambaye inasimamiwa na District Commissioner. Hapo ndipo mahali wananyanyasa wananchi. OCPD wanakutana na DC, Special Branch, hata DO hatakiwi, chifu hatakiwi, Chairman wa County Council hatakiwi, mjumbe hatakiwi. Hwa wakisema tunyanyase huyu, hakuna mtu anaingilia hii Security Team. Kama wewe imekwisha fungwa kwa hawa, utaenda namna hiyo. Hapa sasa tunaomba iwekwe sheria, hata hawa wakikatia mtu lawama kwa huko, na umeenda mpaka kotini na kushinda, unarudi na kustaki DC. Na ukimstaki, tunataka atumie lawyer wake mwenyewe, asitumie yule wa public. Hii inaitwa state council. Na akipatikana na hatia, DC mwenyewe alipe pesa hio. Basi, nafikiri nikimaliza sasa, naungana na sheria hii mimi nataka kuomba, hii sheria ya kulinda wananchi.

Sheria ya kulinda wananchi. Kwa hapa Marakwet, mimi naona kama sheria hio iko kando. Kwa sababu tulipoteza mali chungu nzima, tulipoteza manyumba ya mabati, tulipoteza mashule, tulipoteza watoto, tulipoteza ngombe. Lakini serikalil, hakuchukiwa kama ni disaster. Na Kuangalia na kutoa compensation kwa huyo mtu amepata umaskini kubwa, hakutarajia yeye mwenyewe. Kuna mapendeleo kwa sababu niliona wakati wa Molo, walitoa kitu huko. Wakati wa Laikipia, walilipwa kitu huko. Hata Mt Elgon walilipwa kitu huko, lakini hapa Marakwet, waliwachwa kama si wananchi wa Kenya hii; (in the background) hata Sondwa walilipwa. Lakini hapa Marakwet, tuliachwa! Tunataka sheria ya ku-cover watu wote, na ku-cover Marakwet. Mimi sina ingine, asante.

Com: Domiziano Ratanya: Ngoja hapo Councillor. Ngoja kidogo. Councillor, kuna swali moja ambayo ningetaka ufafanue hapa. Kwa Security team, unasema Chairman ni DC, kuna OCPD na kuna Special Branch Officer, hapo, hukufafanua sawa sawa kama pengine haihitajiki, ama pengine ungetaka wananchi wahusiswe kama Mjumbe ama Councillor, wa hio team, ama haikuwa clear.

Councillor Gablo: Hapa sasa, mimi nilikuwa nataka kama wajumbe wetu wako mbali, ihusishwe kwa County Council Chairman. Na nataka mtu ambaye anachaguliwa na wananchi, si hata clerk; clerk anaweza kushikana na DC tu na kusema hawa ni civil service. Wanashirikiana kwa kunyanyasa. Tunataka sisi tunachagua, halafu akitenda kosa huko, sisi nangojea yeye, na kumwaga, na kumweka mtu mzuri huko.

Com: Domiziano Ratanya: Yaani, mumuonze kwa hiyo team?

Councillor Gablo: Kwa hiyo team ya security.

Com Domiziano Ratanya: OK. Nimeelewa sasa.

Councillor Gablo: Na hata kwa proposal yangu ningetaka Chairman kwa County Council awe Chairman wa Security Team.
(Clapping)

Com Domiziano Ratanya: Asante kwa maoni hayo yako Bwana Councillor Debro. Weka sign yako hapa. Sasa tunaita Anna Chepkien. Ukisikia siwezi kuitamuka, tayari najaribu tu kidogo. Anna yuko? OK Anna ni wakati wako.

Anna Chepkien: Asante sana Bwana Commissioner. Kwa majina naitwa Anna Chepkien. Mimi na simamia kikundi cha Maendeleo ya Wanawake, kwa sababu sisi tumekutana kwa Districts zetu na kujadiliana, kwa maneno ya katiba sisi akina mama, tunataka tupewe

Haki zetu za akina mama. Sikusema akina mama watawale nyumbani, ama watawale mabwana, hapana. Sisi tunatawaliwa kama kawaida, lakini kwa haki yetu, sisi kama akina mama, tumezaa watoto, tumezaa wavulana na wasichana. Na hawa watoto, wameenda shule, wameenda kusoma darasa moja, wameenda secondary, wameenda University, hasa, wakitoka huko, kila mtu amepata degree. Sasa Bwana Commissioner, sisi kwa sisi tunataka haki yetu. Kwa nini wasichana hawapewi cheo kama Directors na zingine? Kwa nini zinapewa tu wavulana? Kila mtoto, alienda darasa, alipata degree kama ya yule mwingine, na wanasema msichana hawezi kupewa cheo kama Director. Na yeye pengine ameshinda hata kijana. Tena wanasema ati pengine wataenda maternity, hata yule kijana, kama yeye ni Director kwa ofisi, siku zingine kama amekuwa mgonjwa, si atakaa hospitali hata miezi mbili halafu anarudi kazini? (laughter) Ni hayo tu Bwana Director, mimi ninaunga ile tulijadiliana na akina mama mkono. Tupewe haki yetu. Asante.

Com: Riunga Kuna swali. Ngoja kidogo Anne.

Com: D. Ratanya: Asante sana mama kwa hiyo pendekezo lako.

Lakini mbali na hiyo, kuna vitu vingine labda unafikiria nyinyi kama akina mama wa maendeleo ati, watoto wetu wa kike wanyanyaswa, na ungetaka turekebishe. Isipokuwa tu tuseme kwa hiyo ma-position makubwa kama Director. Kuna mambo mengine, tuseme kama uongozi, ungetaka kama hao wanawake wetu, wapewe uongozi kama ma-chief, wabunge, watu wengine, na hata President? Anaweza kuwa mwana mke. Nchini zingine wako. Ungetaka tuwapatie viti vingine au tuwasaidie kupata haki zao kwa hizo viti?

Asante sana Bwana Commissioner, mimi, ni getaka hata sisi akina mama, wa hii Constituency yetu, sisi tungepewa hata kuwa Chief, hata Councillor, hata Assistant Chief, na kazi zingine. Hata Agricultural Officer, nani, tupewe hii kwa sababu kila mtu amesoma. Na tunataka hawa watu kama chief, tuwachague kwa mlolongo. Msilete yeye huko tu na pengine mumechagua mtu ambaye amekuja kunyanyasa watu wa nyumbani. Mwenye anatomia tu cheo na hafuati sheria kamili. Asante.

Com: D Ratanya: OK asante sana Anne, ningetaka kuwakumbusha kwamba tulisema kila mtu ana uhuru wa kupeana maoni yake, na kila mtu apewe nafasi. Msipige kelele wakati mtu anasema kitu ama mumwambie sema hivi na hivi. Kwa sababu tunataka kuchukua maoni ya kila mtu. Hayo ni maoni yake. Kwa hivyo tumuheshimu namna hio. OK asante, twende kwa Elias Rotich.

Elias Rotich: Asante sana ma-commissioners wetu. Yale ambayo nilikuwa nimeweka orodha kusema, yamesemwa, na singetaka nirudie sana ninapita juu juu tu. Moja nikuhusu upingamisi hii ambaye imeangamiza wakalejins sana. Mtu akikosa, tuseme kwa mfano ameua mtu, inahusu jamii yote. Kwa hivyo, nafikiri mutatekeleza hio kabisa, kwa makini iwe sheria katika katiba mpya, iondolewe. Hata kwa Mwenyezi Mungu, mtu anabeba msalaba yake, haki yake. Nikimaliza hiyo, nakuja ya pili.

Mishipi yetu iwe katika County Council, hata ingawa kila section inaagalia kulingana na ukoo, lakini iwe katika County Council yetu.

Ya tatu, ni silaha. Wakati Mtukufu Rais alichukua uchukane mapema alitamka kwamba mwananchi yeyote ukiona bunduki mahali popote, julisha serikali. Kwa sababu bunduki hiyo huenda ikatumiwa kukuua wewe mwenyewe. Lakini leo masilaha imesambaswa. Limetambaa kila mahali, na tukipiga ripoti hatuoni hatua ikichukuliwa. Sijui ni nini.

Ya nne, naunga wale wamependekeza majimbo. Majimbo iweko.

Ya tano, nina furaha kusimama mbele ya wakubwa, Commissioners ambayo wanaheshimiwa Kenya hii. Hata Parliament imesongeshwa kwa sababu hamjamaliza kazi yenu. Kwa hivyo nyinyi sio watu wadogo, ni watu wakubwa, na mimi nina furaha.

Ile neno mimi nataka kusema ni hii. Ikiwa Parliament itasongeshwa kwa sababu nyinyi hamjamaliza kazi yenu, ningetaka niseme hivi kwa maoni yangu. Mtukufu Rais ni kiongozi ambaye amefanya mengi sana katika Kenya. Na kwa maoni yangu ningetaka apewe zawadi. Apewe tuzo. Tuzo yake ni hii. Aendeleo kwa miaka mingine tano kama zawadi (clapping) kutoka kwa Wakenya. Kama zawadi ya kupewa na Wakenya. Kwa sababu amefanya mengi. Wacha niseme. Uzuri wa mtu akiwa katika kiketi huonekani. Akisha ondoka, uzuri wake utaonekana. Kwa hivyo kabla hatujasema O Rais alikuwa mzuri, tutambue kama bado angali kiketi kusema ni kiongozi mzuri. Aendeleo kwa miaka mitano. Ikiwa bunge itaongezewa, pia Rais aongezewe. Ma-commissioners, mimi najua kitu kimoja hapa ambaye ni kasoro. Mengi yalifanywa vizuri, lakini tatizo ya marakwet ni vita ya Pokot ambayo imetusumbua sana. Hata mimi nikikaa chini saa hii hakusosi mwilngine atasema nje bwana Secretary wa KANU katika sub branch, wewe unataka miaka iongezwe na tumekwisha, tumeuawa? Tunaomba serikali katika katiba mpya irudishe amani, iwe vile ilikuwa hapo awali. Kwa hayo machache, kwa sababu kila mtu ako na uhuru, yakusema, hayo ni yangu, nimesema. Asante.

Com: D Ratanya: Hebu ngoja kidogo Bwana Rotich kama pengine tuko na maswali, pengine tunayo.

Com: Salome Muigai: Asante sana Bwana Rotich kwa maoni yako. Hii swali la uaji inaendelea kuja, hata jana tulipokuwa Alor swali la mtu kuwa ameua na iwe shida ya mtu binafsi, na sio shida ya jamii nzima. Imeendelea kuja mara kwa mara. Je, ungetaka kutueleza vile ungependa ikuwe kwa katiba mpya?

Elias Rotich: Jambo hilo, ilikuwapo tangu wakati wa babu zetu. Mtu mmoja akiua mtu, kutoka jamii fulani, watu wa yule ameuawa wanavamia ukoo nzima, manyumba yanachomwa, mali inaharibiwa, wengine wanahamishwa, na leo tunafanya maendeleo. Mimi najenga nyumba yangu permanent, ndugu yangu anakosa, nyumba yangu inavunjwa, mimi ninasafirishwa, hali ya uchumi ndio hii imetutatiza, tungetaka serikali uwe sheria. Mtu aatibiwe kulingana na kosa lake.

Asante sana Bwana Rotich lakini kwa sababu naona wewe ni kiongozi hapa, labda ingetusaidia kwa sababu tumesikia sana shida hii la nyinyi Wamarakwet kuvamiwa na majirani wengine. Sijui labda kama uko na mapendekezo fulani- specific proposals ungetaka tuweke, ili kuhakikisha kwamba, shida kama ile ilitikea hapa Marakwet, au mahali pengine Kenya, ungetaka tufanye nini specifically?

Elias Rotich: Ningetaka wanasiasa wawe moja na administration. Ikiwa kuna silaha, katika upande wa Marakwet, hapa na pale, wajibu wetu tukiwa wanasiasa tusiogope, au tisifiche, tueleze serikali, na tuungane na administration mbila kuogopa kusema labda nikifichiwa hii, nitakosa kura kwa wananchi, kwa sababu amani ni kitu ya kipekee. We cannot compare peace with anything else. Kwa hivyo viongozi wote, wa tabaka aina mbali mbali, wawe moja na administration.

Com: D Ratanya: Asante sana Elias kwa maoni yako, andikisha hapo sasa. Joseph Kendagor.

Joseph Kendagor: Asante sana Bwana Chairman, na Commissioners wako wote, Jina langu ni Joseph C Kendagor, retired Town Clerk, wa Eldoret Municipa Council. Bwana Commissioner, nafikiri wacha nianze hivi kwamba, Marakwet Community ni a very marginalized society. Siogopi kusema hivo kwamba, kuna examples nyingi ya kuonyesha kwamba, sisi kama Marakwet, tumesahauliwa sana. Bwana Commissioner, huwezi kuamini kwamba tangu uhuru, 1963, sis community ya Marakwet, hata ingawa tuko watoto ambayo wamesoma, hatujapata DC hata mmoja, tangu 1963. Kuna wengine, wameshapata, wame re-cycle, mtoto mzee amekuwa DC mtoto wake, hata grand child wake amekuwa DC. Sisi hatujaona mtoto wetu wa Marakwet akiwa na hiyo kraoni. Kazi zingine kama MDs

Wa Parastatals, hatujaona. Wewe umeingia katika District hii pengine mara ya kwanza, hakuna tarmac road, vilie vile ni kwamba, kila mtu ambaye amezungumza hapa, ni kwamba marakwet wanauawa, sasa sana, kama experiment na hawa jirani wetu Wapokot. Na serikali inapendelea Pokot. Kwa nini? Wanapatiwa silaha. Wamarakwet, hakuna mtu anakubaliwa kuwa na silaha. Kwa mfano, mashule katika pale, saa zile Wapokot wanavamia, watoto wa Marakwet wanakuja kwa escarpment wanajenga mashule ya shrubs- ya miti miti, ya nyasi, hakuna mtu amefanya harambee, kusema tuwajengee mashule katika hiyo escarpment tu ya mawe, hata kutoa apology, hata kutoa rabi rabi ni shida. Kutoa rabi rabi kwa radio, kutokea wenyewe, hata DC kusema anatoa rabi rabi, ama DC kutoa kwa wale wamarakwet wameuawa, it's a pity. Ni aibu kwa serikali yetu. Ukienda hapa kwa Mancheste, watu wa Markwet wamehama huko, refugees in their own country. Sorry. Ni hayo, make that record, Marakwet maginalized community.

Kuingia kwa memorandum yangu, kwamba tumeandika kwa niaba ya group yetu, tunajiita Ngalantai Welfare Society. Kwa ufupi, tunaomba kwamba tuwe na katibaa ile ambayo inasimamia nchi yetu, inasimamia sisi kama Wanakenya. Ile Katiba ambayo ina guarantee maisha ya binadamu, mali yetu, na iwe katibaa inatusaidia tuwe na amani, tuwe mali, na tuwe na furaha. Kati yetu iwe na Preamble, ya kuamuru wale ambaye wanasimamia, taifa letu, wapate kutumikia sisi kwa njia nzuri. Wapate kutumia mali yetu kufaidhi sisi wenyewe. Nikitoa kwa mfano, katika hapa Marakwet, tuko na, maji, maji kutoka hii nchi yetu, baraka tumepata forests, kuna dam katika Chebara hapa. Hio mali, inatoka nchi ya Wamarakwet. Lakin wamarakwet hawaoni faidha yake. Inatumiwa na wengine. Kati iamuru yakwamba, mali ikitoka mahali fulani, itumiwe kuwafaidhi wenyeji wa huko. Mfano ingine, Maasai wako na wanyama, Mungu aliyo wavariki hawa akawapatia ndovu, akawapatia simba, lakin ile pesa yote inatoka kwa hio, inaenda kujenga high class hotels, in Mombasa and Nairobi, Mt Kenya huko na kutumiwa na wamaasai ku-enjoy the heritage of their property, sorry.

Kitu kingine ni kwamba naungana na wenzangu, kwa nguvu tuwe na serikali ya majimbo. Tunataka serikali iwe karibu na wananchi hawa, wapate kuona serikali iko kwa macho yao. Nasikitika kusema kwamba, pengine civic education hapa ilikuwa very poor, na pengine quality ya presentation ni shallow. Hawana ile indepth of what you require in the constitution. Kwa hivyo tuwe na serikali ya majimbo, ambayo itasimamia vitu kama bara bara, public health, primary education, social services, ziwe katika Provinces.

Citizenship, hakuna mtu awe na citizenship mbili. Tuwe na citizenship moja. Jambo lingine kwamba, umesikia wenzetu wamesema amri za President ni nyingi sana. Tume-propose kwamba tuwe na Ceremonial President, yule ambaye amechaguliwa na raia, asiwe wa chama chochote, yeye ni non-partisan, na awe a symbolic Head of State. Na tuwe na Prime Minister, ambaye kazi yake ni kujibu mambo katika Parliament. Serikali yake ikienda hay wire, anapewa vote of no confidence, anarudi kuchaguliwa tena na raia, ili kurekebisha mambo.

Iko katika katiba yetu 25% ya President. Hiyo, ili President asi shinde tu kwa wingi wa area moja, hio 25% ipate kuendelea. Nimesema kwamba tuwe na Provincial Government. Wqatu wengi wanaogopa, tukizumgumza habari ya majimbo, watu wengine wanatetemeka na tume-propose a safeguard. Tuwe na Commission ambaye tutaita Good Neighbour Commission. Hii Commission itakuwa ikiangalia sheria za kila Province – ya kila majimbo – ama local authority. Wakipitisha kwamba, na kuona hio sheria ni discriminative, wata-propose penalties kwa senate, na kwa kuwa tutakuwa na serikali ya majimbo, tutakuwa na senate. Ile nyumba ya pili katika Parliament. Sasa hii kazi ya Good Neighbour Commission, kila mtu atakuwa apipiga ripoti akiona kwamba amenyanyashwa katika jimbo la Eldoret, basi ako na haki kufanya ripoti. Na commission itachungulia. Itachunguza maneno haya. Vile vile, nimesema tutakuwa na senate, itachaguliwa kutoka kila Province, na kazi yake ni kama ile ya zamani kuangalia sheria za Law House, sheria la Provincial Assemblies, sheria za Local Authorities. Nikiendelea Bwana Commissioner, Members wetu wa Parliament, wanapewa a lot of privileges, mshahara mzuri, minono minono na kuna tabia ambayo imetokea, karibuni kwamba,

Com: D Ratanya: Yes Bwana Kendagor, nitakukatiza kidogo kwa sababu imepitisha dakika yako.

Joseph Kendagor: Yes Sir.

Com: D Ratanya: Kwa hivyo jaribu sasa kumaliza. Tulisema wananchi msisome memorandum. Museme yale ya muhimu, kwa hiyo dakika tano. Lakini wewe ume enda dakika kama tisa, na maliza kwa sababu wewe ni kiongozi.

Joseph Kendagor: Ndio Sir. Namaliza kidogo. Political Parties. Tuwe na sheria, ya kulainisha, viana via siasa. Tuwe na viana vya siasa chache sana. Ziwe mbili au tata, zisizidi tano. Na sheria hiyo, iwe ikiamuru, political parties ziwe ziki-practice internal democracy. Kusiweko na defection every minute. Watu wawe na principles. Mimi nikishindwa katika chama changu leo, nisirudie during the night, na kwenda kwa chama ingine. Tuweko na sheria kwamba huwezi ku-defect within a certain period – say 6 months to the elections or whatever.

La mwisho kwa kuwa nimefanya kazi na Local Authorities, tuwe na very very strong local authorities, ambayo chairman wake, na Mayor wake wamechaguliwa directly na raia. (clapping) Watakuwa answerable, to the public. Na wafanye kazi wakijuwa wakifanya corruption, raia watawafuta. La mwisho vile vile ni kwamba, kuna commissions ziko katika nchi yetu, na ningengeza, tuwe na anti-corruption authority ambayo kila raia, ata-report ile kitu ameona, amedhulumiwa, ameona corruption imefanyika mahali fulani, wanareport. Vile vile, katika nchi zingine kama Tanzania wameanza commission nyingine inaitwa ombudsman. Hiyo vile vile, iingie katika katiba yetu, ili raia wetu wa Kenya wawe na uhuru wa kila aina., kila kona. Ukiangalia mbele, iko nafasi ya ku-report kibaya , ikiangalia kushoto, iko nafasi ya ku-report kibaya. Bwana Chariman, na Bwana Commissioner, ni hayo, yako katika memorandum yangu, nimesema tu kwa ufupi, na nasema ni mzuri,

Com. D Ratanya: Councillor. Ngoja kidogo kuna swali.

Com. Salome Muigai: Asante sana retired Town Clerk, nina swali moja, lenye pengine, sita kutarajia kulijibu wakati huu. Lakin ningetaka pengine ukiwa na nafasi ufikirie. You have can we put to talked at length about marginalization. What concrete proposals reverse either the marginalization, or to put points of redress into it? You have talked about lack of ??? lack of tarmac roads, killings of the ,

Joseph Kendagor: Hata mjumbe wetu wa Parliament, na pana mwingine alikuwako huko, katika areas zingine, it is very painful, utaona baada ya kushindwa kwa Parliamant, kesho he is MD somewhere. Lakini hata mmoja tangu uhuru, Arap Too is sick lakini angalia, yakwamba, hata kupata good pension ili apate kuvaa vizuri, kuliko kuvaa ile viatu zimepasuka. Alikuwa Mheshimiwa hapo Parliament. (clapping)

Com. D Ratanya: OK asante sana Bwana Kendagor kwa Maoni yako, peana hio memorandum. Do you have another

copy? Ama ni hiyo tu? OK , tunaendelea kwa Robert Kipkorir.

Robert Kipkorir: Jina langu ni Robert Kipkorir, Mbunge wa zamani katika Marakwet district. Bwana Commissioners ningependa kuuliza tu kusema, mimi nimeona aibu sana kwa serikali yetu, vile yanaendesha mambo, imekuwa aibu katika Parliament ya sasa. Wakati mimi nilikuwa Mjumbe, mshahara yangu ya kwanza ilikuwa elfu saba. Niliwahi kufanya kazi nyilngi katika Marakwet, kujenga mashule, kutembelea wagonjwa, kusaidia wasiojiweza, na nilifanya kazi mingi. Nimeshangaa vile serikali imesimamiwa siku hizi. Unaona wajumbe wanakula mshahara zaidi ya elfu mia tano, na wnataka kuongezewa uwe miliomi moja, wakati walimu wameuliza mshahara tangu 1997, wanafinywa na inakatazwa. Ukiona mwalimu mmoja anakula mshahara elfu tano., na Mheshimiwa anataka milioni moja, na hawezi kusikizwa. Hii ni aibu. Sis kama viongozi wa marakwet, tunataka ile kitu inaitwa equality. Mishahara ya wafanyi kazi iwe sawa. OK unaweza kupatia Mjumbe zaidi mbele kidogo, kwa sababu anakazi nyingi. Lakini, lazima wale wenye mshahara kidogo waongezewe mshahara, kama walimu, na wafanyi kazi wengine wa serikali. Kwa mfano, umesema polisi wamekuwa corrupt. Mshahara yao elfu tano ni nini katika maisha ya sasa? Na huyu mtu ana watoto katika University, ana watoto katika secondary school, na muna mpatia mshahara elfu tano, si hata huyo mtu akiiba hakuna makosa, kwa sababu hamuangalii masilahi yao (clapping)

Kwa mfano, school fees,

Com. D Ratanya: OK hebu tumpe nafasi. Si hio ndio tulikubaliana? Hebu aseme maoni yake.

Robert Kipkoriri: Kwa hivyo, mimi nataka hio mshahara ya wafanyi kazi kwa jumla, katika wilaya mbali mbali ziwe sawa. Halafu kila mtu anafurahiya. Wakulima walindwe. Kwa mfano, siku moja mimi ninauza mahindi yangu, shilingi elfu mbili kwa gunia. Sasa nauza shilingi mia nne, kwa sababu serikali anakataa kufanya marketing. Wale watu ambao wanasimamia serikali, wanasimamia kazi kama wizara ya planning, hawafanyi kazi zao. Kwa mfano, watu wamekufa katika South Africa kwa sababu ya njaa. Mahindi inatakikana huko. Mahali pengine, chakula inatakikana, lakini sisi tunaulizwa kuuza mahindi yetu kwa shilingi mia nne. Na fertilizers mfuko moja ni shilingi elfu moja mia tano. Mbegu ya kununua, ni shilingi elfu tatu, Mia tatukwa mfuko mmoja. Sasa, mimi ninapata nini katika hio mavuno? Kwa hivyo, mtu anaitwa mkulima amenyanyaswa kabisa. Na amepata hasara kubwa sana. Sisi kama Wamarakwet tuko na viongozi katika area hii, tunalia sana. Kwa hivyo, mtu wa agriculture, aangaliwe maneno yake sawa sawa.

Ningependa tu kuongeza kitu kimoja mwenye kiti, kwamba tumeangalia hii kitu inaitwa security, kweli, hata sikutaka kurudia. Kuna kitu tunasema katika Parliament, Sessional paper number 1, katita mbunge, sheria ya kulinda watu na mali yao. Kwa mfano, wale Wamarakwet wamekuwa massacred katika Chesungut, what we have said is the worst thing is walikufa. Wamewacha watoto yatima.

Kwa nini hawa watoto serikali haiwezi chukua na kuwasomesha mpaka wafikishe miaka 18 au mpaka 21 halafu inawachilia? (clapping) Kwa nini tusingaliwe namna hio? Watoto wa hawa watu wameachwa, sasa wamekuwa maskini, wanatembea,

wamekuwa “chokora”. Watoto wa watu ambao walikuwa na mali yao, walikuwa na utajiri. Hiyo ni kusema nini Bwana Mwenye kiti? Sisi tunataka very seriously, security. Na hatutaki mchezo kwa hiyo maneno. Kama sivyo, tutangaze vita. Wamarakwet, musikubali kuwa mzigo kwa serikali! Twende tukachukuwe silaha na kuua watu wengine. Hii ni aibu sana. (laughter) OK, hiyo imekwisha, lakini nilikuwa nataka kurudia kitu kidogo tu katika mambo ya forestry. Kidogo tu.

Kuko namna hii Bwana Mwenye kiti; katika Marakwet community, sisi tunaheshimu sheria ya kwetu, kinyumbani vile wababa zetu walikuwa wanatuendesha. Forests zikawa kwa clans. Na hizo forests, mimi siwezi kutoka clan ingine, kwenda kuingia katika forest ya mtu mwingine. Ni kama mashamba. Na ilikuwa inalindwa, na wazee, na hakuna mtu alikuwa anaingilia. Halafu after independence, 1964 Mwenye kiti, 1963, wakati tulipata uhuru, serikali ikanyanganya wananchi powers. Na wakachukuwa, na wakaanza kusema inalindwa na Central Government. Kutoka haapo, wakaleta wageni, kwenda kulinda hio forests. Wale wageni wakaenda huko, wakaanza kufieka forests. Wakanyakua. Unaona mtu anaitwa forest officer, anasimamia forest, unakuta iko na ngombe mia moja ndani ya forest. Na kusema hii ni mali yangu, nimepata. Unaenda huko, unaambia mzee. Anakwambia, wewe ishi hapa, nitakukatia plot hapa. Sasa forest yetu inavamiwa kutoka pande zote. Ile mambo ya clans iliharibika. Kwa hivyo sisi tunataka irudi katika County Council, na wananchi wenyewe, warudie mambo yao, ya kuangalia mbuzi zao. (clapping) Hii maji ambayo iko Chebara sasa ni uchungu sana kusikia Directors wa hio maji, ni watu foreigners katika area hio. Hakuna Mumarakwet hata mmoja amepolekwa huko akawa Director. Watu wote wale employees, wale wanafanya kazi, hata wale wakufieka chini hata wale hawaja soma ni watu wa wengine. Hakuna Wamarakwet huko! Sisi tunataka 85% to 90% wawe Wamarakwet. Wale watu wanafanya kazi katika hio Dam (clapping) Basi kwa mambo ya distribution, umeshasikia hiyo, kwamba Wamarakwet wamenyanyashwa. Haya, nimesema mambo ya marketing. Na sasa Bwana mwenye kiti kuna kitu kinaitwa culture ya watu. Kama ni Wakikuyu, wako na culture yao. Kama ni Wamarakwet, wako na culture yao. Kwa nini tusiheshimu culture yetu? Sisi tunaletewa culture ya wazungu kwa nini? Unavaa trousers, kwa nini bibi yangu anavaa trousers? Kuna aja gani bibi yangu kuvaa trousers? Mimi nataka bibi yangu avae marinda mzuri, anaka kama mama wa nyumbani hata wazazi wangu aonyeshe heshima akiwa mbele ya wazazi wao. Sisi hatutaki hii aibu inaletwa na foreigners. Halafu wanakuja kuharibu culture yetu. Mama yangu na baba yangu mpaka leo wana heshima. Wanafuata kimila na wanaita mimi mtoto, na kuita wale wajukuu, tunakaa vizuri.

Hii maneno ya kuchanganya culture ni mbaya. Mimi sio mzungu, mimi ni mwafrika, na mimi ni Marakwet. Na mimi lazima nikae kama Mumarakwet (clapping). Haya mwenye kiti, mimi nataka kukueleza kwa ufupi,

Com. D Ratanya: OK sema ya mwisho kwa sababu dakika zako zimekwisha.

Robert Kipkorir: Kuna shamba inaitwa White Highlands ambayo wazungu walinyanganya sisi. Na wakati wazungu waliondoka, wakasema tumeondoka, lakini hii shamba, tilinyanganya Wamarakwet, na hii tulinyanganya wakikuyu, basi, Wakikuyu walirudishiwa upande yao. Wamarakwet hawakurudishiwa yao. Sisi tulifukuzwa katika Trans Nzoia, mpaka Ua-sin-gishu. Takafukuzwa na Wazungu. Sasa kutoka 1963, watu walitoka mahali pengine wakavamia hizo mashamba. Na

sisi tukanyimwa kwa maana walikuwa kwa ppower siku hizo, mpaka sasa, sisi tunaishi kwa male, na Uasingishu ni kwetu. Munanyanyasa watu namna hii, na hii shamba iko Trans Nzoia yote, chini tunapakana na watu wa Elgon na tunapakana na Wabukusu, na barabara ya mpaka yetu ilikuwa kupita rami ya Kitale mpaka Eldoret. Sasa kabila zingine zinakuja mpaka hapa hata Kapcheloti, yote imeenda. Sasa hii shida tutaishi namna gani Brwana Mwenye kiti? Sisi tunataka mashamba yetu turudishiwe, watu waondike katika hiiuo trans-zoia waende kwao.

Com. D. Ratanya: OK, Mheshimiwa ngoja kidogo, pengine kuna swali.

Com. Salome Muigai: Asante sana Bwana Mheshimiwa kwa maoni yako, mimi nina swali moja kwako. Umesema kuwa umezungumaia kwa kirefu habari ya mila zetu. Mimi swali langu ni hili. Mila inakomaa ama mila inaendelea ikibakilika kama vile sisi na wewe tumeenda tukibadilika. Wakati mwingine tulivaa mavazi nimetupatia lugha tofauti, zimetupatia, je tinataka lugha yenye itakubakiana na kubadilika na nyakati, ama mila ni kitu kilichokufa kama aa kama hii, inaitwaje? Mawe; yenye haibadiliki ama ni kitu chenye kiko alive and able to change with time.

Joseph Korir: Mimi nataka Bwana Mwenyekiti ningependa

Tu mila ya watu iheshimiwe, yaani kama kwa mfano, kama watu wameshasoma wasome lakini wajue kwamba wa Marakwet historia yao ilikuwa namna gani, ili mambo yetu kama kimila isipotee. Kama sasa, kwa mfano ee kwa desturi vile wazee wetu walikuwa wanakaa, nataka iwe recorded, katika vitabu ijulikane tulikuwa tunakaa namna hii. Hata kama tumepaa, sisemi lazima tukae kama zamani. Nina sema hiyo kazi yetu iwe retained na iwe iendeshwe yaani kwa kisasa, yaani iendeleo kama ya kisasa lakini iwe kama Marakwet au vile tunakaa. Tusikae kama wazungu. Tukae kama Wamarakwet lakini iwe modernized. Mumenielewa hapo? Tafadhali na tusipoteze kazi yetuikatwe namna hii, halafu tuone tulikiwa na watu walikuwa wanaitwa Marakwet na kazi yao ilikuwa namna hii na hakuna. Hatutaki namna hio.

Com. D Ratanya: Mheshimiwa hapo tumeelewa. Nashukuru sana kwa maoni ile unapeana. Kama una memorandum yako upeane na u-sign register yetu. Aa sasa twende kwa Lena Kilimo Kilimo. Lena Kilimo sasa ni wakati wako.

Lena Kilimo Kilimo: My name is Lena Kilimo Kilimo, most of what I would have wanted to say has been presented through Maendeleo ya Wanawake, because we want on together collecting our views and we have a memorandum. To register a few things, I want to highlight especially as I sar down there, I want to talk about equality.

Equality has to do with equal opportunities and more so to my fellow Marakwet who are seated here. Equal opportunities, I would like to address the men to educate your child, the girl and the boy. Do you educate your firl to just become a housewife or to just work? We know we would in equality retain our sole biological role and even the congenital role, matrimonial role, we shall retain. But equality which we want to put in our constitution is equal opportunities to be respected. Equal respect, the respect they would give to a DC man, they should they should to a decent woman, so that to remove the cultural stereo types

which we really have in the past in our cultures that women are not considered as people. They are considered as children or people who do not easily make up their mind.

But education has taught us to be able to make up our minds so we want equal opportunities and to all our Marakwet men here, equality is equal opportunities. Bringing Beijing home does not mean I have brought Beijing so that I can rule over you. It means only that bringing Beijing home there is a role, it has to do with education that I have had and out there I do my role as a leader of the community or anything that I have but congenital, matrimonial home rules will be retained. So I hope I am clear on that one when we come to equality.

I come from the valley where most of the land is trapped land and all the community people know that our boundaries is from this stone to that stone because that is what we use to demarcate. We would like in the new constitution that the trust land should have a title saying this is trust land, this piece of land from this stone or from this hill to this hill belongs to this community.

Whoever in the future is to be demarcate to those people in that community or not, it will at least ensure the security of that land that it belongs to those people, and not as it is now that it belongs to the government and they can do anything with it.

About national dress if we have to have a national dress, may be the design at which it will be made, will just be different so we are for the idea that we should have a national dress if it is the same colour, it is the same colour; but if it is a man's, it will be tailored in a way that it should fit a man. And it should be tailored to fit into a woman. So that we can remove that which men think women are supposed to be flowers there, for decoration, or you use us to show off your national dress and the men should show off our national dress. So we can remove that negative attitude of women being used as models of some sort.

Security: we would like it to be put in the new constitution – where it is known that there is conflict, between two ethnic communities then the security arm of the Government, should lead in the boundary – the no man's land. They should be able to clear and live in the boundary. For example, in the Kerri Valley now, OK the government ensures that we have security, but where do these security men live? They live along the road and where we are killed or where our animals are taken, it before you reach the road; they finish us before you reach where the personnel is. So I think to curb that personnel problem, if you have heard, every body else is talking about it, I would like from my own contribution that there should be a boundary, a clear no man's land where the security personnel live. So that they know who is crossing in who's side. I would also like the aggressors to be treated as bandits by the security. If the security has been located on Market side, and they see people coming, to kill us from the Pokot side, how come when they arrive they say we are waiting for orders from above so that we can effect or whether we can arrest that person or shoot? So we would like the security personnel, if they are on the Marakwet side, they should take themselves as Marakwets. That time they should not be as the Government but as Marakwets and so they are protecting themselves from any aggressors and they should be given the authority to shoot anybody who has aggressed them. Like wise on the Pokot side, if we go to that side, then they are protecting the Pokot side. In that

way, we might remove the security problem.

Another one is on education. Because of poverty, many of us are not able to take our children to school but if the Government can give us free education, and free equipment, especially in the primary, then I would work so hard and save money to educate my child in secondary but after secondary, we would like the Government to take over. Right now, we have so many school leavers who are hanging around playing pool, if it is put in the constitution that, OK the Government will educate your child up to standard 8, for the next 4 years or so try to make sure you educate that child and after form 4 the Government should take these children to the Youth Service where they are given skills. Whether I got A or I got B, we go to the institution, like the youth service, we are taught skills, then from there, my brother or sister, who got A can go to University and me who had D, I will have got some skills that can enable me to earn a living after that, and that one should be free so that all of us can at least have a skill on how to survive.

Another one is to do with the MPs, we just want to elaborate that those who want to vie for Parliament, should not be allowed to dish out money. If they want, they can build a school, contribute to the school, or community project and if they are known to have dished money at some point, then they should be disqualified. They should not be cleared to run.

Another one we would like in the new constitution is the separation of the powers. If you are an MP we want you to remain an MP, and not to become a member of the cabinet, so that if we send an MP with our grievances, he can talk boldly to the Government, the executive and the cabinet who are not supposed to be MPs. We wonder how some body who is supposed to be a Minister will run his ministerial duties and at the same time know what is happening in his grass root home.

The people who form the Cabinet should be professionals who are may be elected by Parliament and not an MP who may be just got there and is put in the cabinet. They can never discharge their duties in the constituency well, or accuse the Government for neglect of security. If my MP is the Minister of Security, and his people are killed, and we tell him, “go and tell the Government that you have killed us” whom is he going to ask? Is he going to ask himself why have you killed the Marakwets? So we would like those ones to be removed.

NGOs: NGOs should be removed. We know that the work of NGOs is really to alleviate the lives of the community. But sometimes we have NGOs who do not involve the local people. We have so may NGOs in Nairobi who are operating saying that we are working in the Rift Valley, we are working where, but really, the person who is getting hurt does not get those services. They just write proposals, that money comes, but they are theoretical but not practical. My suggestion is that if any NGOs has to be given a certificate to operate as an NGOs it should be in the local, and it should involve the people from the local area, and their office should be in that locality whether they walk up to there without a vehicle.

For the disabled people, we would like to have an institution for the disabled people in every district so that as a woman I will

not be ashamed of having a disabled child as I know this is a child of the Government. Immediately we recognise the disability of the child, we take them to that institution and the Government takes care and gives them the skills so that they can survive later in life. It should be a place where I can go and visit that child as a parent. Thank you very much.

Com: D Ratanya: Thank you very much Lena Kilimo, just wait, may be we have questions to ask you.

Com: Salome Muigai: Thank you very much, that was very elaborate sharing, I have a few questions. I want to start with children with disabilities. Why should our children with disabilities be the responsibility of the Government yet our other children are our own responsibility? What is the right of the child with disability to the family? I do appreciate that it could be more expensive than the other, but I also would like to see the role of the family towards the child with disability. The other question that I would want to ask you is on the role of women as leaders. At present we have not – a lot of women as we went round, some women had told us that until women are given quarter system, we don't please request you to stop the – (excuse me, ningekuomba uwache habari ya soda kwanza tuasiliane na huyu mama - asante.) We have been told that unless women get a quarter system of getting into governance, it will be very very difficult to make a breakthrough. So we have had some places where we have been even told to have affirmative action, and we have heard all those types of suggestions. I would like you to share with me how you see the Marakwet woman making her break through in leadership. What are the strategies that you would like to see in place? Thirdly, and lastly, I would also like to ask you about the girl child because not only aren't women joining leadership, but, yesterday, we were told in a role that all impediments to the girl child, even at finishing primary school, being able to go to a secondary school where sometimes parents make choices and sent the boy child to school before the girl child, we were also told about early marriages and all that. So I want you to share with us your thoughts on the way to remove some of those impediments along the way constitutionally, so that this girl child has got an equal chance to reach leadership and to reach maturity, and to reach education as her brother. Those are many questions. I will remind you as we go along. That I started with the child with disabilities.

